

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

MKOA WA NJOMBE

Simu: 026-2968833

Faksi: 026- 298832

E- mail: td@njombetc.go.tz

njombetc@gmail.com

Tovuti: www.njombetc.go.tz



**S.L.P 577,
NJOMBE.**

20/07/2017

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anawatangazia Wananchi wote kuwa kesho 21/07/2017 kutakuwa na mkutano wa Mwaka wa Baraza Kuu la Madiwani litakalofanyika katika Ukumbi wa halmashauri ya Mji Njombe uliopo katika Mtaa wa Lunyanywi Kata ya Mji Mwema kuanzia saa nne kamili za asubuhi.

Ikumbukwe kuwa Mkutano huo ni Mkutano wa kufunga Baraza kuu La Madiwani kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na litatoa tathmini na mafanikio ambayo Halmashauri ya Mji imefikia kwa kipindi cha Mwaka Mmoja ambapo taarifa za utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri zitawasilishwa.

Wananchi Wote Mnakaribishwa.

Imetolewa Na,

Afisa Habari,

Halmashauri ya Mji Njombe.